# 16 za Uanaharakati 2024

## Ahidi Tena! Wajibika! Wekeza Rasilimali Kuzuia!

## Bangili ya Urafiki: Bangili: Ni Alama ya Vuguvugu Letu

Mbali na uanaharakati kwa njia ya Utepe wa Zambarau, Bangili za Urafiki zinaweza kuashiria kujitoa kwetu katika kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake. Kutengeneza bangili za urafiki kunatuwezesha kujieleza kupitia ubunifu wetu. Wakati wa kipindi cha kampeni, unaweza kutengeneza na kutoa bangili za urafiki kwa wanaharakati wanaoendesha vuguvugu katika jamii yako ambao wamejitoa kuunga mkono lengo letu kuu la kujenga dunia isiyo na Ukatili. Tendo hili la mshikamano ni udhibitisho kwamba hatuko peke yetu katika kufanya kazi hii, na kwamba kila mmoja wetu ana jukumu muhimu katika safari hii. Pata nafasi ya kuwatambua na kusherehekea ili kujenga na kuendeleza vuguvugu letu na kudumisha kujijali kwa pamoja.

## Maelekezo:

1. Kata kipande cha uzi baada ya kupima urefu wa mzunguko juu ya kifundo cha kiganja cha mkono wako. Acha nafasi ya ziada, inaweza kuhitajika!
2. Funga ncha moja ya uzi. Hakikisha fundo ni kubwa kuliko shimo lililopo kwenye shanga-hii inamaanisha kuwa unaweza kufunga mafundo kadhaa.
3. Kuwa mbunifu! Shanga unazoziona ziko za rangi na herufi mbalimbali. Je! ni mtindo gani unaweza kutengeneza kwa kutunga shanga kwenye uzi? Unataka kutumia rangi za aina ngapi? Ikiwa una mtu unafikiria kumpa bangili, je, ni rangi gani anaweza kuzipenda? kuna neno linaloweza kuwakilisha nia ya kujitoa kwao, shukurani zako, au matumaini wanayoleta kwa wengine?
4. Endelea kushona shanga na uziongeze hadi utengeneze bangili ya kutosha kuzunguka juu ya kifundo cha kiganja cha mkono wako.
5. Funga fundo baada ya kushona ushanga wa mwisho, hakikisha kwamba shanga zimekaza vizuri na haziwezi kudondoka kwenye kamba.
6. Funga ncha mbili za kamba kwa pamoja. Sasa una bangili ya kupendeza sana!
7. Toa zawadi ya bangili kwa mtu anayekutia moyo kupitia kazi yake ya kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake, pata muda wa kuwaeleza kwa nini unawapa bangili hizo. Waalike muweza kushirikishana kile kinachowapa motisha wa kuwa pamoja, mnaweza kubunga bongo juu ya mawazo yenye ubunifu kwa ajili ya kuendeleza ushirikiano!

Tunatumani umefurahia mchakato mzima wa kutengeneza na kushirikishana. Tunakuhimiza kufanya mambo yanayoweza kuwaunganisha na wadada wenzeko wakati wowote katika kipindi cha mwaka mzima.

Raising Voices
16 DAYS
GBV Prevention Network
Building Momentum•Fostering Activism